Toleo Na. 06

# USAFIRI ARDHINI

ISSN 2961 - 6255 Januari - Machi, 2025



# LATRA YAWAKABIDHI POLISI VIPIMA ULEVI 3,050 ILI KUIMARISHA USALAMA BARABARANI

## LATRA YATOA ELIMU KWA MADEREVA NA WAMILIKI WA PIKIPIKI WILAYA YA SAME KILIMANJARO

"LATRA imewaletea jambo jema ambapo kwa umoja wenu mkiungana mnaweza kuunda chama cha ushirika (SACCOS) kitakacho wainua kiuchumi kwa kurudisha asilimia ishirini ya mapato mnayokusanya kuleta LATRA serikali imeleta fursa na mnapaswa kuzichangamkia"

Bw. Salum Pazzy.

Uk 7

## WATUMISHI LATRA WAASWA KUONGEZA UBUNIFU

"Niwasihi kuongeza ubunifu katika maeneo yenu ya kazi na muendelee kutoa huduma bora kwa wateja huku mkitekeleza majukumu yenu kwa uweledi, uadilifu na ufanisi kwa kuzingatia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001, na mjitathmini mnapokuwa kazini kuwa unamchango gani kwenye idara yako,

CPA Habibu Suluo

Uk 15

# TAHARIRI



**CPA HABIBU JUMA SULUO**
Mkurugenzi Mkuu - LATRA

Kwa mara nyingine nakukaribisha mdau na msomaji wa Jarida la USAFIRI ARDHINI katika toleo la sita lililosheheni taarifa lukuki zinazohusu jitihada za Serikali zinazotekelezwa na Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika kuboresha sekta yako ya usafiri ardhini nchini kuanzia mwezi Januari hadi Machi, 2025.

Jarida hili linaandaliwa mahususi ili kukuhabarisha kuhusu kazi, majukumu, huduma mbalimbali zinazotolewa na LATRA, udhibiti wa huduma za usafiri ardhini pamoja na matukio mbalimbali yanayohusu sekta ya usafiri ardhini, lengo ni kuhakikisha tunakuwa na uelewa wa pamoja wa shughuli zote zinazotekelezwa na Mamlaka kwa uwazi na hatimaye kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Tarehe 15 Januari mwaka huu, tulitembelewa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ikiongozwa na Mhe. Moshi Selemani Kakoso (Mb), Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambapo ilifanya kikao na Menejimenti ya Mamlaka. Kamati iliipongeza Mamlaka kwa jitihada za kubuni na kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) iliyoongeza ufanisi, kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za usafiri ardhini kwa uwazi na haraka.

Pia, tumeendelea kuboresha ushirikiano na kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kuendesha shughuli za kiudhibiti kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Kufanikisha hili, Februari 27, 2025 Bodi ya LATRA ilifanya kikao kazi cha pamoja na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA) iliyopo Unguja – Zanzibar. Kikao hiki kimetuleta pamoja na kupata fursa ya kubadilishana uzoefu wa maeneo yetu tunayoyadhibiti kwa sababu Mamlaka hizi mbili zinafanya kazi zinazoshabihiana.

Vilevile, kwa kipindi hiki tumewafikia wadau wetu kwa kuwapatia elimu na kuwakumbusha kufanya kazi zao kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini ili kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Sambamba na hili, tumeendelea kuwasihi madereva wa vyombo vya moto kibiashara kote nchini kujisajili na kuthibitishwa na LATRA kama illivyoainishwa kwenye Kanuni ya (4)(1) ya Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu ya mwaka 2020.

Kwa sasa naweka nukta ili upate fursa ya kusoma kwa kina yote tuliyokuandalia kwenye Jarida hili la USAFIRI ARDHINI ili kufahamu vizuri maendeleo na udhibiti wa sekta ya Usafiri Ardhini nchini. Kwa maoni yoyote usisite kuwasiliana nasi kwa namba zetu bila malipo 0800110019 / 0800110020 au kupitia Mfumo wa e- mrejesho unaopatikana kwa anwani https://emrejesho.gov.go.tz/ au kwa kufika ofisi ya LATRA iliyo karibu yako

*Nakutakia usomaji mwema*

*"Pamoja kwa Usafiri Bora"*

# KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YAPONGEZA MATUMIZI YA MIFUMO LATRA



*Mhe. Moshi Selemani Kakoso (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu akiwa kwenye kikao kati ya LATRA na kamati hiyo Januari 15, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Mhe. Moshi Selemani Kakoso (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa jitihada za kubuni na kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayorahisisha utoaji wa huduma za usafiri ardhini nchini.

Mhe. Kakoso amesema hayo kwenye kikao kati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Wizara ya Uchukuzi, LATRA na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), kilichofanyika Januari 15, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Nawapongeza kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na ninawasihi muendelee kutumia mifumo hiyo ili kuepusha rushwa na kuongeza ufanisi katika shughuli zenu za udhibiti na hii itaendelea kuleta tija na kuboresha zaidi sekta hii ya usafiri ardhini," alisisitiza Mhe. Kakoso.

Naye DCP Johansen Kahatano, Kaimu Mkurugenzi Mkuu LATRA, alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za udhibiti usafiri ardhini kwa Kamati hiyo, alisema kwa kutambua umuhimu wa TEHAMA, Mamlaka inatumia mifumo mbalimbali ikiwemo Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) uliosaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto za ajali nchini.

"VTS imeunganishwa kwenye vichwa vya treni na mabasi na hadi mwishoni wa mwezi Desemba, 2024 jumla ya mabasi 11,551 na vichwa vya treni 18 vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo wa VTS. Kati ya vichwa hivyo, 16 ni vya Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) na viwili (2) ni vya Shirika la Reli Tanzania (TRC). Kuwepo kwa mfumo huu kumeimarisha shughuli za udhibiti wa mwenendo wa udereva njiani kwa muda wote na mahali popote vyombo hivi vilipo. Pia, uwepo wa mfumo huu umesaidia udhibiti wa mwendokasi baada ya Serikali kuidhinisha mabasi kusafiri kwa masaa

**Inaendelea UK 2 >>>**

## KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YAPONGEZA MATUMIZI YA......

*<<< Inatoka Uk 1*

yote 24 hapo mwezi Oktoba 2023," amesisitiza DCP Kahatano.

Vilevile amesema kuwa, mbali na kutambua mwenendo wa gari, LATRA imeweka teknolojia ya utambuzi wa madereva wanaoendesha mabasi muda wowote kwa kutumia kitufe cha utambuzi (i-Button) kabla ya kuanzisha safari.

Pia, DCP Kahatano ameeleza kuwa, mwaka 2023/2024, LATRA imewezesha abiria kuona mabasi yakiwa barabarani kupitia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System ama PIS) unaopatikana kwa anwani ya pis.latra.go.tz uliounganishwa na VTS ambapo abiria anaweza kufuatilia taarifa za basi analosubiri ama analosafiri nalo kwenye simu yake kupitia mfumo wa PIS ambapo ataweza kufahamu nauli, muda wa kuwasili kituoni na mwendokasi akiwa safarini.

Vilevile amebainisha mfumo mwingine kuwa ni Mfumo Jumuishi wa Tiketi Mtandao ambapo LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Bima (TIRA) na sekta binafsi (wamiliki wa mabasi na watoa huduma binafsi wa tiketi mtandao) ilianza kazi ya kuunda mfumo jumuishi wa tiketi za kielektroniki kwa mabasi ya abiria mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024.

"Mfumo jumuishi utaunganishwa na mifumo binafsi ya wamiliki wa mabasi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wasafiri, kupata takwimu sahihi za watumiaji wa huduma na kuondoa changamoto ya wapigadebe kwenye vituo vya mabasi na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma," ameeleza.

DCP Kahatano ameitaja mifumo mingine inayotumiwa na LATRA ni Mfumo wa Kusajili Wahudumu na Kuthibitisha Madereva (DTS), Mfumo wa Kutoa Leseni (RRIMS) pamoja na Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA APP)

> **"Nawapongeza kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na ninawasihi muendelee kutumia mifumo hiyo ili kuepusha rushwa na kuongeza ufanisi katika shughuli zenu za udhibiti na hii itaendelea kuleta tija na kuboresha zaidi sekta hii ya usafiri ardhini,"**
>
> **Mhe. Moshi Kakoso (Mb)**



# LATRA NA ZARTSA ZABADILISHANA UZOEFU WA KIUTENDAJI



*Bodi ya Wakurugenzi na baadhi ya Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakiwa kwenye kikao cha pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA) Februari 27, 2025 ukumbi wa Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto, kwa Silva (Dole- Zanzibar)*

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ikiongozwa na Prof. Ahmed Mohamed Ame imefanya kikao cha pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA) inayoongozwa na Bw.Mkadam Khamis Mkadam, Mwenyekiti wa Bodi hiyo kwa lengo la kuboresha ushirikiano pamoja na kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kuendesha shughuli za kiudhibiti kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Akizungumza wakati wa kikao hicho kilichofanyika ukumbi wa Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto, kwa Silva (Dole-Zanzibar) Februari 27, 2025, Prof. Ame amesema kuwa LATRA na ZARTSA ni Mamlaka zinazofanya kazi zinazoshabihiana na hivyo ili kuboresha shughuli za uendeshaji na usimamizi wa huduma za usafiri ardhini, ni muhimu kwa taasisi hizo kuwa na ushirikiano mzuri na maono yanayoendana.

“Lengo kuu la Bodi ya LATRA kuja hapa katika kikao hiki cha mashirikiano ni kuendeleza ushirikiano ambao tulishauanzisha na pia kujifunza masuala kama vile Sheria iliyoanzisha ZARTSA na Sheria nyingine za Kisekta, kufahamu utaratibu wa utoaji wa leseni za vyombo vya moto mnavyovidhibiti pamoja na masharti yake pamoja na kufahamu utaratibu wa ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto,” amefafanua Prof. Ame.

Naye Bw. Mkadam, Mwenyekiti wa Bodi ya ZARTSA ameeleza kuwa,kikao hicho ni chenye tija kwa taasisi zote mbili ambapo itaandaliwa hati ya maelewano (Memorandum of Understanding) itakayoongeza ushirikiano mzuri na itakayoondoa changamoto kwa wadau wa usafirishaji wa pande zote mbili yaani Tanzania Bara na Zanzibar na hatimaye kunufaika na huduma bora za usafiri ardhini.

Kwa upande wake, Bw. Haji Ali Zubeir, Mkurugenzi Mkuu wa ZARTSA amesema kuwa, LATRA na ZARTSA zitaendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali ikiwemo utoaji wa mafunzo kwa madereva wa vyombo vya moto vinavyodhibitiwa ili kuongeza uelewa wa matumizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usalama barabarani pamoja na kutii Sheria bila shuruti,

Naye, CPA Habibu Juma Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA ameeleza kuwa LATRA inatumia mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayorahisisha utendaji kazi, utoaji huduma kwa wananchi pamoja na udhibiti kwa jumla.

“Sisi tumetengeneza Mfumo wa Tiketi za Kielektroni ambapo kwa sasa tiketi za mabasi yote ya masafa marefu zinapatikana kwa njia ya mtandao. Tumeruhusu watoa huduma kutengeneza mifumo yao na sisi tunaisajili na imeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa hiyo kodi ya Srikali haipotei. Mfumo pia unatoa orodha ya abiria waliosafiri na taarifa zao muhimu na wakati wowote tukihitaji tunaingia kwenye

*Inaendelea UK 4 >>>*

## LATRA NA ZARTSA ZABADILISHANA UZOEFU WA KIUTENDAJI

*<<< Inatoka Uk 3*

mfumo. Kwa bahati nzuri tumeingia makubaliano na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambapo wakati wowote ikitokea dharura ni rahisi kwao kuingia kwenye mfumo na kufahamu nani alikuwepo safarini na kutoa stahiki kwa mujibu wa taratibu zilizopo", amefafanua CPA Suluo

> **tumetengeneza Mfumo wa Tiketi za Kielektroni ambapo kwa sasa tiketi za mabasi yote ya masafa marefu zinapatikana kwa njia ya mtandao.**
>
> **CPA Habibu Suluo**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA ni taasisi ya umma iliyo chini ya Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA) ipo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na taasisi zote mbili zimedhamiria kuendeleza ushirikiano ili kuleta mapinduzi chanya kwa sekta zinazodhibitiwa na hatimaye kila mdau wa usafiri wa ardhini kwa pande zote mbili aweze kunufaika kwa huduma bora zinazotolewa na taasisi hizi kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

# LATRA YATANUA WIGO WA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

DCP Johansen Kahatano, Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), amesema kuwa Mamlaka imetanua wigo wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi, kwa kuanzisha njia mpya za usafiri wa umma katika maeneo ya miji na kuzifanyia mapitio njia za zamani kwa kuzirefusha au kuzifanya za mzunguko, pia imeanzisha njia mpya hususan zinazounganisha Jiji la Dodoma na maeneo mengine ya nchi.

DCP Kahatano amebainisha hayo alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za udhibiti usafiri ardhini kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu katika kikao kilichofanyika Januari 15, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ameongeza kuwa, Mamlaka imeendelea kutekeleza shughuli za kiudhibiti kwa ufanisi katika Usafiri wa Barabara, Usafiri wa Reli pamoja na Usafiri wa Waya.

Alizungumzia jukumu la utoaji wa Leseni na usimamizi wa masharti yake kwa upande wa usafiri wa barabara, amesema huduma za Usafiri wa barabara zimeimarika ikiwemo kuongezeka kwa maombi ya leseni za usafirishaji katika njia mpya na zilizokuwepo ambapo idadi ya leseni za usafirishaji iliongezeka kwa jumla ya asilimia 42 kutoka leseni 230,253 katika mwaka wa Fedha 2020/21 hadi

> **"Tumeanza kutoa elimu ya vyama vya ushirika na kuhamasisha vijana waendesha pikipiki kujiunga katika vyama vya ushirika na kupewa uwakala wa LATRA"**
>
> **DCP Johansen Kahatano,**

*Inaendelea UK 5 >>>*




*DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara akimkabidhi zawadi Mhe. Moshi Selemani Kakoso (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu baada ya kikao kati ya LATRA, na Kamati hiyo Januari 15, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

## LATRA YATANUA WIGO WA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

*<<< Inatoka Uk 4*

kufikia leseni 326,576 katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

"Sekta imeonesha kuimarika kutoka katika athari za UVIKO-19 zilizojitokeza mwaka 2020/21 na 2021/22 ambazo zilisababisha huduma zinazoombewa leseni kuongezeka kwa kiwango kidogo katika miaka hiyo. Athari zilionekana katika Sekta ya utalii na biashara ambazo ni miongoni mwa wadau wakubwa katika soko la usafiri na usafirishaji. Kufikia mwaka 2022/2023, leseni za huduma ziliongezeka kwa asilimia 18 na mwaka 2023/2024 zikaongezeka kwa asilimia 15 kulinganisha na asilimia 4 kwa mwaka 2021/2022, ambapo katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2020/21 hadi 2023/24 jumla ya leseni 1,080,940 za usafirishaji kwa njia ya barabara zilitolewa," ameeleza DCP Kahatano.

Vilevile amesema, Mamlaka imetekeleza maelekezo ya Serikali ya kuanzisha na kusimamia huduma za mabasi kwa saa 24, "Utekelezaji huu ulianza tarehe 1 Oktoba, 2023 kwa kutoa masharti mahsusi kwa watoa huduma waliomba ratiba za kufanya safari za usiku. LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tumeendelea kusimamia huduma hizi ambazo zimeonekana kuwa ni chaguo la wananchi wengi lenye tija ya matumizi ya muda wa mchana kwa shughuli za uzalishaji, gharama za kulala njiani na utulivu wa safari".

Akizungumzia pikipiki za magurudumu mawili na matatu amesema, "Tumeanza kutoa elimu ya vyama vya ushirika na kuhamasisha vijana waendesha pikipiki kujiunga katika vyama vya ushirika na kupewa uwakala wa LATRA. Zoezi hili linaenda vizuri na tayari mkoa wa Kilimanjaro una chama (KIBABOT) na unafanya vizuri".

DCP Kahatano alisema LATRA imeendelea kudhibiti huduma za usafiri wa reli ambapo katika reli ya kisasa (SGR) Mamlaka iliidhinisha nauli za abiria kwa huduma za kawaida mwezi Juni 2024 ambapo kati ya Dar-es-Salaam na Dodoma ni Shilingi 31,000 kwa daraja la

*Inaendelea UK 6 >>>*

## LATRA YATANUA WIGO WA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

*<<< Inatoka Uk 5*

kawaida na Shilingi 50,000 kwa huduma ya haraka katika daraja la kawaida.

Kwa upande wa usafiri wa waya, ameishukuru Wizara ya Uchukuzi kwa kuandaa rasimu ya Kanuni za udhibiti wa usafiri huo ambazo zimeshawasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kupokea maoni yao. Usafiri wa waya hutumika katika maeneo yenye milima na vivutio vya utalii kama Arusha na Kilimanjaro. Hii ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii nchini ambapo kwa sasa idadi ya watalii imeongezeka.

Naye Mhe. Moshi Selemani Kakoso (Mb) ambaye ni mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu alipongeza jitihada zilizofanyika na ameitaka Mamlaka kufuata na kutekeleza maoni ya wajumbe yaliyotolewa katika kikao hicho ili kuendelea kuboresha huduma za sekta ya usafiri ardhini nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)

# MADEREVA DODOMA WAASWA KUSAJILIWA NA KUTHIBITISHWA NA LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewaasa madereva wa vyombo vya moto kibiashara kujisajili na kuthibitishwa na LATRA kama illivyoainishwa kwenye Kanuni ya (4)(1) ya Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu ya mwaka 2020.

Hayo yamebainishwa na Bw. Ezekiel Emmanuely, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dodoma alipotoa elimu ya uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu kwa madereva wa magari maalum ya kukodi (Special hire) jijini Dodoma Februari 07, 2025.

"Ni kosa la kisheria kuendesha basi bila kuthibitishwa na Mamlaka, hivyo nitoe wito kwa madereva na wahudumu wa mabasi Tanzania kutii Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufika ofisi za LATRA zilizo karibu yao kwa ajili ya kuthibitishwa na kusajiliwa", amesema Bw. Ezekiel.

Naye Bw. Humphrey Ngweta, kiongozi wa Ulinzi na Usalama wa magari maalum ya kukodi jijini Dodoma amesema, "Naishukuru LATRA kwa kutufuata eneo letu la kazi na kutupatia elimu hii na hivyo niwaombe madereva wenzangu kujitokeza kwa wingi ofisi za LATRA ili tufanye kazi zetu kwa misingi ya Sheria zilizowekwa kuepuka kuchukuliwa hatua," ameeleza Bw. Hamphrey

Kwa upande wake Bw.Yusuph Lukungu, dereva wa magari maalum ya kukodi anaeleza tija ya elimu aliyoipata na kumpelekea kuhamasika kusajiliwa na LATRA katika kituo chake

*Inaendelea UK 7 >>>*



*Bw. Ezekiel Emmanuely, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dodoma (watatu kushoto) na akitoa elimu kwa madereva wa magari maalum ya kukodi kuhusu uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara Februari 07, 2025 Jijini Dodoma.*

## MADEREVA DODOMA WAASWA KUSAJILIWA NA KUTHIBITISHWA NA LATRA

*<<< Inatoka Uk 6*

cha kazi jijini Dodoma.

"Kujisajili sio suala gumu kama nilivyokuwa nafikiria cha msingi uwe na cheti chako cha chuo ulichosomea, kitambulisho chako cha NIDA pamoja na leseni yako, jambo hili nimelikamilisha leo, na ninaishukuru sana Serikali kupitia LATRA kwa jitihada ya kuhimiza madereva kujitokeza kwa wingi kusajiliwa ili kuheshimisha kada udereva hapa nchini," amesisitiza Bw. Lukungu.

Serikali imeweka nia thabiti ya kuitambua kazi nzuri inayotekelezwa na madereva wa vyombo vinayodhibitiwa na LATRA, hivyo suala la uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu linaenda kuipa thamani tasnia ya udereva pamoja na kuwaongezea wigo wa ajira kwa kuwa cheti cha uthibitishaji cha LATRA kinatoa fursa kwa madereva kupata ajira ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

## LATRA YATOA ELIMU KWA MADEREVA NA WAMILIKI WA PIKIPIKI WILAYA YA SAME KILIMANJARO

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imetoa elimu kuhusu kazi na majukumu ya LATRA, ukataji wa leseni za LATRA kwa pikipiki za magurudumu mawili pamoja na Usajili wahudumu na uthibitishwaji wa madereva kwa wadau wa usafirishaji hususan Madereva na Wamiliki wa Pikipiki za Magurudumu Mawili, katika vituo mbalimbali vya bodaboda wilayani Same - Kilimanjaro Februari 4, 2025.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu Bw. Salum Pazzy Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA ameelezea umuhimu wa kuwa na leseni za LATRA kwa wasafirishaji hao pamoja na kuunda vyama vya Ushirika (SACCOS) kwa wanachama hao.

"Ukataji wa leseni za LATRA ni takwa la kisheria ndio maana LATRA tumesogeza huduma wilayani hapa, vile vile LATRA imewaletea jambo jema ambapo kwa umoja wenu mkiungana mnaweza kuunda chama cha ushirika (SACCOS) kitakacho wainua kiuchumi kwa kurudisha asilimia ishirini ya mapato mnayokusanya kuleta LATRA serikali imeleta fursa na mnapaswa kuzichangamkia" ameeleza Bw. Pazzy.

Aidha Bw. Frank Sanga kaimu afisa mfawidhi LATRA Wilaya ya Same-Kilimanjaro, ameelezea tija ya LATRA kuwa na ofisi Wilayani hapo ambayo imeleta tija kubwa kwa kuhamasisha madereva na wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili juu ya ukataji leseni za LATRA na kuelezea jinsi ambavyo ofisi ya LATRA Wilaya ya Same inashirikiana na jeshi la polisi wilayani hapo.

"Kwa sasa madereva na wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili wanajitokeza kwa hiari kuja kukata leseni za LATRA ishara ambayo inaonyesha muamko na mwanga kwetu LATRA lakini pia tunashirikiana kwa karibu na jeshi la polisi, hawa ni wenzetu na hata ukimkuta bodaboda amekiuka taratibu na kupita eneo lenu la ukaguzi ukimwomba askari, huwa anamsimamisha na tunampa elimu" amefafanua Bw. Sanga.

Naye Bw. Amos Alfred katibu wa madereva wa pikipiki za magurudumu mawili kituo cha bodaboda halmashauri ya wilayani Same - Kilimanjaro ameipongeza LATRA kwa kufika kwenye kituo hicho na kutoa elimu hususan kuwa wakala wa utoaji wa leseni za LATRA.

"Kituo kama hiki kinaweza kuwa wakala wa ukataji wa leseni za LATRA ambacho kinaweza kutoa huduma kwa niaba ya LATRA lakini pia kuleta ukaribu wa huduma

*Inaendelea UK 8>>>*




*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA (wa kwanza kushoto) akiwaelekeza jambo baadhi ya Madereva na Wamiliki wa Pikipiki za Magurudumu Mawili katika vituo mbalimbali vya bodaboda Wilayani Same - Kilimanjaro Februari 4, 2025.*

## LATRA YATOA ELIMU KWA MADEREVA NA WAMILIKI WA PIKIPIKI WILAYA YA SAME KILIMANJARO

*<<< Inatoka Uk 7*

kwa waendesha pikipiki za magurudumu mawili ambao wapo kwenye kituo hiki na vituo vingine "ameeleza Bw. Alfred.

Vilevile Bw. Chedieli Mgonja ameishukuru na kuipongeza LATRA kwa kufikisha elimu wilayani same na jinsi ambavyo mwitikio wa madereva wa pikipiki za magurudumu mawili umebadilisha mtazamo wao juu ya LATRA na kupata uelewa wa faida za kukata leseni ya LATRA na kuunda vyama vya Ushirika.

"Tunaishukuru sana LATRA kwa kutuelewesha faida ya kukata leseni za LATRA kwa sababu ni leseni ambayo tunakata kwa ajili ya kubeba abiria lakini pia tunashukuru maana wametupa elimu ya kwamba tunaweza tukafungua vikundi na kutengeneza ushirika wetu wa bodaboda na tukakata leseni zetu LATRA na kufaidika na asilimia inayotoka LATRA kwaio ikatunufaisha kwa kupata kiasi na kutuinua kiuchumi kwa kupitia mfumo huu" amefafanua Bw. Mgonja

Mchakato wa uanzishwaji wa Vyama vya ushirika (SACCOS) kwa wamiliki na madereva wa bajaji na bodaboda nchini kote ni mpango wa Mamlaka uliolenga kuwakwamua kiuchumi wanachama wa vyama hivyo huku wakiwa na dhima kubwa ya kujidhibiti wao wenyewe.

**LATRA imewaletea jambo jema ambapo kwa umoja wenu mkiungana mnaweza kuunda chama cha ushirika (SACCOS) kitakacho wainua kiuchumi kwa kurudisha asilimia ishirini ya mapato mnayokusanya kuleta LATRA serikali imeleta fursa na mnapaswa kuzichangamkia"**

**Bw. Salum Pazzy**



CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akimkabidhi IGP Camilus Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini vipima ulevi 3, 050 kwa lengo la kuimarisha usalama Barabarani Januari 6, 2024 Makao Makuu ya Polisi Jijini Dodoma.

Wanawake wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa kwenye Maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani viwanja vya Leaders Club Dar es Salaam Machi 8, 2025.






Bw. Nelson Mmari Afisa Mfawidhi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Tabora akitoa elimu kuhusu matumizi ya Mifumo yakiudhibiti inayotumiwa na Mamlaka ikiwemo Mfumo wa Taarifa Kwa Abiria (PIS) Februari 11, 2025 Mkoani Tabora.

# LATRA YAASWA KUEPUKA RUSHWA



*Bw. John Shija, Afisa Mchunguzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) akiwaasa watumishi wa LATRA katoa elimu ya Rushwa katika kikao cha Sita cha Baraza la Wafanyakazi la LATRA, ukumbi wa Mikutano wa Ngorongoro Crater, Jijini Arusha Januari 24, 2025.*

Bw. John Shija, Afisa Mchunguzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) amewaasa watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kuzingatia uwazi na uwajibikaji pindi wanapotekeleza majukumu yao.

Bw Shija amebainisha hayo Januari 24, 2025 alipowasilisha mada ya Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mkakati wa Utekelezaji Awamu ya Nne (NCSAPIV) 2023-2030 katika kikao cha Sita cha Baraza la Wafanyakazi la LATRA kinachofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ngorongoro Crater uliopo katika Jengo la Ngorongoro Jijini Arusha.

Ameeleza kuwa, suala la uwazi kuhusu utaratibu wa kupata huduma za LATRA ni muhimu kwa kuwa, wadau watakuwa na ufahamu wa jinsi ya kupata huduma hizo na hivyo kupunguza mazingira yanayoweza kuashiria mianya ya rushwa, "kufanikisha hili, matumizi ya mifumo ya TEHAMA yatasaidia kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mwananchi hatolazimika kukutana na mtumishi pindi anapoomba hadi anapopata huduma anayoitaka hivyo endeleeni kubuni na kuhamasisha matumizi ya mifumo kwenye huduma zenu".

Ameongeza kuwa, kila mtumishi anapaswa kuwajibika ipasavyo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo na kufahamu athari za ukiukwaji wa taratibu hizo. Pia, ni muhimu watumishi kupatiwa elimu ya maadili na athari za rushwa mahala pa kazi ili wanapotekeleza majukumu yao, wafahamu madhara ya kujihusisha na vitendo hivyo.

"Ili tuweze kuwa na utekelezaji bora wa Mkakati huu, watumishi tunao wajibu wa kutojihusisha na vitendo vya rushwa na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu, hivyo Baraza la Wafanyakazi linawajibika kuhamasisha watumishi mahala pa kazi kuzingatia Maadili na kuchukia Rushwa ili kuleta ufanisi katika

*Inaendelea UK 11 >>>*

## LATRA YAASWA KUEPUKA RUSHWA

*<<< Inatoka Uk 10*

utekelezaji wa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (NACSAPIV 2023-2030)," ameeleza.

Pia, Bw. Shija amebainisha madhara ya Rushwa kuwa ni kuchelewesha utoaji wa haki kwa wananchi, kuzorota kwa maendeleo ya nchi, kukithiri kwa maovu, kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa, kupunguza uwajibikaji, na kadhalika.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, rushwa ni adui wa haki, hivyo kila mtumishi anapaswa kuchukia vitendo vya rushwa, ukizingatia huduma za Mamlaka zinamgusa kila mtu nchini na hivyo watumishi wawe waadilifu wanapotekeleza majukumu ya Mamlaka siku zote.

"Mtumishi wa umma lazima uwe wa kuaminika, hivyo ni wajibu wa kila mtumishi kupinga na kupambana na vitendo vya rushwa ili kuongeza uadilifu mahali pa kazi, kuwa na utumishi wa umma ulio bora na wenye tija na hatimaye kuleta maendeleo ya taasisi na nchi kwa jumla," ameeleza CPA Suluo.

Baraza la Wafanyakazi la LATRA linaendesha vikao vyake mara moja kwa mwaka na linajumuisha Wajumbe wa Menejimenti, Wawakilishi wa Watumishi wa Idara na Vitengo, Maofisa Wafawidhi wa Mikoa yote pamoja na Uongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania – COTWU (T)- Tawi la LATRA.

# LATRA YAWAKABIDHI POLISI VIPIMA ULEVI 3,050 ILI KUIMARISHA USALAMA BARABARANI

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura amesema Jeshi la Polisi limeweka mikakati madhubuti ya kudhibiti ajali za barabarani ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyokuwa akiyatoa mara kwa mara ya kuhakikisha ajali za barabarani zinadhibitiwa ipasavyo.

IGP Wambura ameyasema hayo wakati akipokea vifaa 3,050 kati ya 10,000 vya kupima ulevi kwa madereva vilivyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ambapo CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA alikabidhi vifaa hivyo katika hafla iliyofanyika Makao Makuu ya Polisi Jijini Dodoma Januari 6, 2024.

IGP Wambura alisema kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani watakuwa wakali kwa madereva wazembe ambao wamekuwa wakisababisha ajali za barabarani ambapo pia wataendelea kutoa elimu ili kuhakikisha kuwa watanzania wanakuwa salama.

"Tumeweza kuzuia uhalifu wa aina mbalimbali na sasa nguvu pia tunazielekeza kwenye usalama barabarani kwa kuwa takwimu za ajali bado zipo juu hivyo ni lazima tuwe wakali sana ili kuona

*Inaendelea UK 12 >>>*

> **"Tumeweza kuzuia uhalifu wa aina mbalimbali na sasa nguvu pia tunazielekeza kwenye usalama barabarani kwa kuwa takwimu za ajali bado zipo juu hivyo ni lazima tuwe wakali sana ili kuona sheria za usalama barabarani zinafuatwa"**
>
> IGP Camillus Wambura

# LATRA YAWAKABIDHI POLISI VIPIMA ULEVI 3,050.....

*<<< Inatoka Uk 11*

sheria za usalama barabarani zinafuatwa ili kuokoa maisha ya Watanzania" alisema IGP Wambura.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA Habibu Suluo amesema, utendaji kazi wa LATRA unahitaji sana ushirikiano kutoka Jeshi la Polisi ambalo ndilo lenye dhamana ya kusimamia Sheria za Usalama Barabarani na hivyo vipima ulevi hivyo vitasaidia Kikosi cha Usalama Barabarani katika kudhibiti ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva walevi na wazembe pindi wanapokuwa barabarani na kuendesha pasipo kuzingatia sheria.

CPA Suluo alisema uwepo wa vifaa hivyo utasaidia kupima madereva mara kwa mara wawapo barabarani jambo ambalo litasaidia kufanya barabara zetu kuwa salama.

Aidha alisema LATRA itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutumia mifumo katika kufanya ukaguzi wa magari ambapo kwa sasa wanaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika maeneo mbalimbali.

Hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo ilihudhuriwa na Makamishna wa Polisi, Manaibu Kamishna wa Polisi, baadhi ya Makamishna Wasaidizi Waandamizi wa Polisi na Maofisa kutoka LATRA



*Jeshi la polisi nchini wakiwa kwenye hafla fupi na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakijadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya usafiri ardhini baada ya Jeshi la Polisi kukabidhiwa na LATRA vifaa 3,050 vya kupima ulevi kwa madereva wa vyombo vya moto kibiashara, Januari 6, 2025 Makao Makuu ya Polisi Jijini Dodoma*

# LATRA YAPONGEZWA MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA



*Bw.Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano - LATRA akieleza kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka kwa kamati ya siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Mchafukoge Februari 3, 2025 ukumbi wa Mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam.*

Mhe. Jamal Abubakar, Mwenyekiti wa Kamati ya siasa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Mchafukoge ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kuendelea kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini.

Mhe. Jamal amesema hayo kwenye kikao kati ya Kamati ya siasa CCM Kata ya Mchafukoge na LATRA kilichofanyika Februari 3, 2025 ukumbi wa Mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam.

"Nawapongeza sana kwa jitihada mnayofanya kwa kutumia mifumo ya TEHAMA kwakuwa imeongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yenu kwani mnafanya vizuri katika kusimamia sekta ya usafiri na kuhakikisha huduma zinakuwa bora kwa wananchi," amesema Mhe. Jamal.

Katika kikao hicho Bw.Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ameielezea mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na LATRA katika utekelezaji wa majukumu yake ambayo imerahisisha utoaji huduma kwa wasafirishaji na wananchi.

"Miongoni mwa mafanikio tunayojivunia ni Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ulio rahisisha ufuatiliaji wa mwenendo wa dereva anapokuwa safarini na kupunguza ajali za barabarani pia Mamlaka imerahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi kupitia Mfumo wa PIS (Mfumo wa Taarifa kwa Abiria) unaomuwezesha abiria kufahamu taarifa za mabasi yanayowasili katika vituo vya mabasi nchini na mwendokasi wa basi," ameeleza Bw. Pazzy.

Aidha Bw. Pazzy ameitaja mifumo mingine kuwa ni, Mfumo Tumizi wa LATRA App unaomuwezesha mwananchi kufahamu nauli zilizoidhinishwa na LATRA, pamoja na kuhakiki uhai wa leseni, Mfumo wa huduma kwa wateja ambao unatumiwa kuwasiliana na wateja moja kwa moja siku zote kupitia namba bila malipo 0800110019 au 0800110020.

*Inaendelea UK 14 >>>*

## LATRA YAPONGEZWA MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA

*<<< Inatoka Uk 13*

Vilevile amesema LATRA inajivunia utoaji wa huduma za safari za saa 24 zilizoanza kutolewa rasmi tarehe 1 Oktoba, 2023 nakuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Kwa upande wake Bw. William Masai, Afisa Leseni na Usajili LATRA ameieleza kamati hiyo kuwa, LATRA inafanya kila jitihada kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa mjini zinazotolewa na daladala ili kuweza kuwafikia watanzania mbalimbali.

"Kupitia elimu mbalimbali na ukaguzi endelevu tunaendelea kuboresha huduma za usafiri wa daladala na kutatua changamoto mbalimbali za usafiri huu na tumeweza kuweka idadi maalum katika njia mbalimbali ili kurahisisha huduma za usafiri nchini," amesema Bw. Masai.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 10 akiwemo Mhe. Mariam Lulida, Diwani Kata ya Mchafukoge pamoja na Baadhi ya maafisa kutoka LATRA.

## SP MAGAYANE AWAONYA MADEREVA WANAOCHEZEA MFUMO WA VTS

SP Peter Magayane, Mkuu wa kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tabora amesema kuwa, endapo dereva atabainika kuchezea na kuharibu Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) wanapokuwa barabarani hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Amebainisha hayo hivi karibuni kwenye ziara ya mafunzo ya siku mbili ya namna Mfumo wa VTS unavyo fanya kazi, alipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari- VTS na Stendi Kuu ya Mabasi Magufuli Jijini Dar es salaam.

"Niwatahadharishe madereva ambao wanatabia ya kuchezea ving'amuzi vinavyofungwa kwenye mabasi kuwa waache mara moja tabia hiyo, na watambue kuwa wakija Mkoa wa Tabora wajue kwamba wanaenda sehemu ambapo kuna wataalamu ambao wameshapata elimu ya kutosha kuhusu Mfumo wa VTS na dereva yoyote atakayechezea Mfumo huu ajue kabisa atakutana na mkondo wa Sheria," amesema SP Magayane.

Vilevile Bw. Emmanuel Aloyce, Msimamizi wa mifumo kutoka kampuni ya ICT PACK ambaye ametoa mafunzo ya Mfumo wa VTS anaelelezea umuhimu wa mfumo huo na kuwa ndio Mfumo mama wa Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaomuwezesha abiria kupata taarifa za mabasi yanayowasili kituoni.

*Inaendelea UK 15 >>>*



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA (aliyesimama) akielezea jinsi Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unavyofanya kazi kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tabora wakiongozwa na SP Peter Magayane, Mkuu wa kikosi hicho (aliyeketi wa kwa nza kushoto) Februari 26, 2025 Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari- VTS kilichopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam.*

## SP MAGAYANE AWAONYA MADEREVA WANAOCHEZEA MFUMO WA VTS

*<<< Inatoka Uk 14*

"Kwenye ziara hii nimepata nafasi ya kuelezea namna Mfumo wa VTS unavyofanya kazi na namna ya kutambua viashiria vya mfumo uliochezewa kwa vitendo, mfumo huu wa VTS ndio Mfumo mama unaowezesha upatikanaji wa taarifa kwenye Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unapatikana kupitia anuwani ya www.pis.latra na kinga'muzi cha VTS kikichezewa hata mfumo wa PIS hautotuma taarifa kwa usahihi," ameeleza Bw. Aloyce.

Wakati huohuo CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amepongeza jitihada zinazofanywa na kikosi cha Usalama Barabarani kutoka Tabora na kuongeza kuwa kituo cha mabasi Nzega kinakwenda kuwa kituo rasmi cha mabasi ili kutatua changamoto za usafiri wanazokutana nazo na kuahidi kurahisisha upatikanaji wa Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) katika stendi hiyo.

"Kituo cha Nzega kitakwenda kuwa kituo rasmi na mabasi yote yanayopita eneo hilo lazima yaingie pale na tutaweka runinga itakayoonesha Mfumo wa Taarifia kwa Abiria kama tulivyoweka stendi ya Magufuli Dar es Salaam na Stendi ya Mabasi Nanenane iliyopo Jijini Dododoma na abiria wataweza kupata taarifa za mabasi yanayowasili katika kituo hicho," ameeleza CPA Suluo.

LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama barabarani wamejipanga kuhakikisha huduma za usafiri zinakuwa bora na salama hapa nchini.

---

# WATUMISHI LATRA WAASWA KUONGEZA UBUNIFU

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewaasa watumishi wa idara ya barabara inayoongozwa na DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA kuongeza ubunifu na juhudi katika kutekeleza majukumu yao,

Amesema hayo Februari 28, 2025 alipofungua rasmi Mkutano wa Idara ya Udhibiti Usafiri wa Barabara uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Magadu Mess, Mkoani Morogoro ukiwa na lengo la kupata mrejesho wa utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichopita, kufanya tathmini ya utendaji kazi wa idara hiyo na kuweka mikakati ya pamoja ili kuboresha utendaji kazi na kufikia malengo ya Mamlaka.

"Niwasihi kuongeza ubunifu katika maeneo yenu ya kazi na muendelee kutoa huduma bora kwa wateja huku mkitekeleza majukumu yenu kwa uweledi, uadilifu na ufanisi kwa kuzingatia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001, na mjitathmini mnapokuwa kazini kuwa unamchango gani kwenye idara yako, tutumie akili zetu kuwa

*Inaendelea UK 16 >>>*

> **"Tutumie akili zetu kuwa wabunifu kuleta mabadiliko chanya kwenye kazi zetu tusiogope kuzungumza, ubunifu ndio mwanzo wa mapinduzi ya maendeleo kwenye kazi,"**
>
> CPA Habibu Suluo

## WATUMISHI LATRA WAASWA KUONGEZA UBUNIFU

*<<< Inatoka Uk 15*

wabunifu kuleta mabadiliko chanya kwenye kazi zetu tusiogope kuzungumza, ubunifu ndio mwanzo wa mapinduzi ya maendeleo kwenye kazi," amesema CPA Suluo.


Kwa upande wake DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA ameeleza kuwa, kukua kwa sekta ya Usafirishaji imechagizwa na maboresho yanayofanyika kwenye sekta hiyo ikiwemo ushirikishwaji baina ya wadau na matumizi ya mifumo katika utendaji kazi.

"Maboresho ya teknolojia kwenye mifumo ya usafirishaji ya LATRA yamerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wakati ikiwemo Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS), ambao kwa sasa unamuwezesha msafirishaji kupata leseni kiganjani mwake bila haja ya kufika ofisi za LATRA, Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS), Mfumo Tumizi wa LATRA App, na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)," amesema DCP Kahatano.

DCP Kahatano ameongeza kuwa, taswira ya Mamlaka kwa wadau wa usafirishaji inazidi kuwa bora kwa jinsi Mamlaka inavyookaa na kuzungumza na wadau hao, na LATRA ipo kwa ajili ya kuwahudumia wao ili kuboresha zaidi sekta ya usafirishaji nchini.

Naye Bi. Mwadawa Sultan, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria LATRA amewafahamisha watumishi kuhusu mwongozo wa Kanuni na Sheria za Mamlaka katika kutekeleza majukumu ya idara ya Barabara. "Katika kikao hiki tumeweza kujua na kuelewa zaidi Sheria za Mamlaka hususan kifungu cha 5 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini sura ya 413 ambayo ndio Sheria iliyounda LATRA na kimsingi inatupa jukumu la kutekeleza Sheria za kisekta," amesema Bi Sultan.

Mkutano huo umefanyika Februari 28 hadi Machi 1, 2025 na umejumuisha wajumbe wa menejimenti ya LATRA na maafisa wote walioko chini ya idara ya Barabara LATRA kutoka mikoa yote Tanzania Bara. Mkutano huo umewawezesha maafisa hao kubadilishana uzoefu na kujadili mada mbalimbali ikiwemo mfumo mpya wa ukataji tiketi kwa njia ya mtandao SAFARI TIKETI na Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) ambapo inatajwa kurahisisha utendaji kazi za kiudhibiti.



# CPA SULUO AWASIHI WATUMISHI WA LATRA KUTOA HUDUMA BORA KWA WATEJA



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akizungumza na watumishi wa idara ya barabara wakati akifungua rasmi Mkutano wa Idara hiyo uliofanyika ukumbi wa mikutano wa Magadu Mess, Mkoani Morogoro, Februari 28, 2025*

CPA Habibu Juma Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi watumishi wa Mamlaka kutoa huduma bora kwa wateja huku wakitekeleza majukumu yao kwa uweledi, uadilifu na ufanisi kwa kuzingatia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001.

CPA Suluo amesema hayo Januari 24, 2025 alipofungua rasmi Kikao cha Sita cha Baraza la Wafanyakazi la LATRA kinachofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ngorongoro Crater uliopo katika Jengo la Ngorongoro Jijini Arusha kwa lengo la kupata mrejesho wa utekelezaji wa maazimio ya kikao cha mwaka 2024, kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Mamlaka, kujadili mipango mipya ya Mamlaka, kuweka mikakati ya pamoja ya kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka pamoja na kufahamiana na kuongeza umoja kama wanafamilia ya LATRA.

CPA Suluo ameeleza kuwa, ni wajibu wa kila mtumishi kumjali mteja kwa kumhudumia kwa furaha na kuzidi matarajio yake ili kupunguza malalamiko na hatimaye kujenga taswira chanya kwa wateja wa Mamlaka.

“Kwa sasa tupo katika mchakato wa kupata uthibitisho wa Kimataifa wa huduma tunazozitoa yaani ISO Certification, hivyo ni muhimu sisi sote tutoe huduma zetu kwa wateja kwa kiwango cha kimataifa tukiweka wazi taratibu za upatikanaji wa huduma zetu huku tukifuata Kanuni na miongozo tuliyojiwekea,” ameeleza CPA Suluo.

Katika michakato ya uandaaji wa Mipango na Bajeti za Mamlaka, CPA Suluo amesisitiza suala la ushirikishwaji wa watumishi katika maamuzi ya mipango inayowahusu pamoja na uandaaji wa bajeti ya Vitengo au Idara zao ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na umiliki wa taarifa muhimu za uendeshaji wa taasisi kwa jumla.

Pia, amewaasa watumishi wa LATRA kufanya kazi kwa umoja, upendo na ushirikiano ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa kuwa kila mtumishi ana

***Inaendelea UK 18 >>>***

## CPA SULUO AWASIHI WATUMISHI WA LATRA KUTOA HUDUMA BORA KWA WATEJA

*<<< Inatoka Uk 17*

mchango wake katika kufikia dira ya Mamlaka.

Mawasilisho yaliyotolewa katika kikao hicho ni Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mkakati wa Utekelezaji Awamu ya Nne (NCSAPIV) 2023-2030, Uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa Ngazi ya Taasisi, Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001 pamoja na Marekebisho ya Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024.




# MADEREVA PIKIPIKI NA BAJAJI WATAKIWA KUFUATA SHERIA

Madereva pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda), Pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) na Pikipiki za kubeba mizigo (Maguta) Wilaya ya Korogwe wametakiwa kufuata Sheria za usafiri ardhini nchini ili kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Hayo yameelezwa na Bi. Gloria Sanga, Afisa Tarafa Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga aliyemuwakilisha Mhe. William Mwakilema, Mkuu wa Wilaya ya Korogwe kwenye kikao kazi cha kutoa elimu ya kazi na majukumu ya LATRA kwa wadau wa usafirishaji kilichoendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Wilaya ya Korogwe, Mkoani Tanga Februari 05, 2025.

“Ni jukumu lenu kuzingatia Kanuni na kufuata Taratibu za usafirishaji hususan kuwa na leseni za LATRA pamoja na kutojihusisha kwenye vitendo vihalifu kwa kuwa mmepewa dhamana ya kubeba maisha ya watu na mkisababisha ajali zitagharimu maisha ya binadamu,” amesema Bi. Sanga.

Naye Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha

*Inaendelea UK 19>>>*

> **“Ni jukumu lenu kuzingatia Kanuni na kufuata Taratibu za usafirishaji hususan kuwa na leseni za LATRA pamoja na kutojihusisha kwenye vitendo vihalifu kwa kuwa mmepewa dhamana ya kubeba maisha ya watu na mkisababisha ajali zitagharimu maisha ya binadamu,”**
>
> Bi. Gloria Sanga

## MADEREVA PIKIPIKI NA BAJAJI WATAKIWA KUFUATA SHERIA

*<<< Inatoka Uk 18*

Uhusiano na Mawasiliano kutoka LATRA amewataka wasafirishaji kuzingatia elimu waliyoipata ili kuongeza uelewa katika utekelezaji wa Kanuni, Sheria na Taratibu za leseni za usafirishaji.

"Mamlaka imewapatia elimu hii ili kuongeza mwamko wa ukataji leseni za LATRA na mnapaswa kufuata Sheria za nchi ili kuepuka athari za kutofuata Sheria. Na Serikali imepitisha Kanuni za Usafirishaji za mwaka 2024 ambapo imeruhusu ushirika kwa wasafirishaji unaolenga kuongeza wigo wa ukataji leseni za LATRA na asilimia ishirini ya mapato mtakayopeleka LATRA yatarudishwa kwenye ushirika wenu," amesema Pazzy.

Kwa upande wake, ASP Richard Muwe, Kaimu Mkuu wa Usalama Barabarani – Korogwe amewasihi wadau hao kujiunga na Vyama vya ushirika (SACCOS). "Mjitokeze kwa wingi kupata elimu, mshikamane wala msirudi nyuma na mchangamkie fursa hii ya kuunda Vyama vya Ushirika itakayoleta tija katika kujikwamua kiuchumi pia niwakumbushe kuwa jukumu la ulinzi na usalama kwa wilaya yetu ni jukumu letu sote," amesisitiza ASP Muwe.

Bw. Masoud Mohamed, Afisa Mfawidhi ofisi ya LATRA Wilaya ya Korogwe amesema ofisi hiyo imesogeza karibu huduma za usafiri ardhini kwa wasafirishaji na wadau kwa jumla ukizingatia Korogwe ni sehemu rahisi kufikika kutoka Wilaya zingine kama Lushoto na Handeni na hivyo imerahisisha udhibiti wa huduma za usafiri na usafirishaji.

Wakati huohuo, Bw. Alinani Ateli, ameishukuru LATRA kuwapatia elimu ya kuunda vyama vya ushirika, "Umoja wa Bajaji Wilaya ya Korogwe, ni wakataji wazuri sana wa leseni za LATRA, na nawashauri wenzangu wa pikipiki za magurudumu mawili pamoja na Pikipiki za kubeba mizigo maguta nao waingie kwenye ukataji wa leseni hizi ili tunapounda Chama chetu cha Ushirika basi kikawe ni Chama chenye nguvu na manufaa kwetu sote," amesisitiza Bw. Ateli.

Kikao kazi hicho kilihudhuriwa na wadau wa usafirishaji wapatao 100 wakiwemo madereva na wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda), magurudumu matatu (Bajaji) na Pikpiki za kubeba mizigo (Maguta) pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Wilaya ya Korogwe na Maafisa wa LATRA.



*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA akitoa elimu kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka kwa wadau wa usafirishaji Wilaya ya Korogwe, Mkoani Tanga Februari 05, 2025.*

*Mha. Hanya Mbawala, Aliyekuwa Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) (wa kwanza kulia) akiongoza ukaguzi wa mabehewa ya kubebea mizigo na makasha ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) stesheni ya reli Ruvu Februari 25, 2025.*






*Bw. Jerive Malaki, Afisa Mwandamizi Usajili wahudumu na Uthibitishaji wa Madereva Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akitoa elimu ya usajili na uthibitishaji wa madereva wa malori wa kampuni ya Usangu Logistiki Machi 13, 2025 Ofisi za kampuni hiyo Jijini Dar es Salaam.*

*Bw. Emmanuel Ezekiel, Afisa Mfawidhi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Dodoma akitoa elimu ya Uthibitishaji na Usajili wawahudumu wa magari maalumu ya kukodi (special hire) na ukataji wa leseni za LATRA kwa pikipiki za magurudumu mawili jijini Dodoma Februari 7, 2025.*



# LATRA YAPONGEZWA KWA KUSOGEZA HUDUMA KARIBU NA WADAU



*Bw. Amani Mwakelebela, Afisa Mfawidhi LATRA ofisi ya Wilaya Ifakara (aliyesimama wa katikati) akitoa elimu ya Uthibitishaji wa madereva na Usajili wa wahudumu kwa madereva na mawakala wa mabasi ya masafa marefu Wilayani hapo Februari 06, 2025.*

INSP Blandina Kasongwa, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kufungua ofisi mji wa Ifakara ambayo imeongeza tija kwa kutatua changamoto mbalimbali za usafiri na usafirishaji kwa wadau usafiri ardhini.

INSP Kasongwa amesema hayo Februari 06, 2025 Wilayani Kilombero ambapo LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabani, walitoa elimu ya Uthibitishwaji wa madereva na Usajili wa wahudumu kwa madereva na mawakala wa mabasi ya masafa marefu mji mdogo Ifakara Wilayani hapo.

"Kipindi hatuna ofisi za LATRA kwa hapa Ifakara kwa kweli palikuwa na changamoto kubwa sana na wasafirishaji wengi hawakuwa na leseni za LATRA, lakini baada ya kusogezewa huduma karibu, mtu mwenye changamoto na dharura yoyote, LATRA imekuwa ikitatua changamoto izo kwa urahisi na haraka, na kimsingi LATRA kufungua ofisi Ifakara imepunguza ajali wilayani hapa kwa kuwa magari yote lazima yafanyiwe ukaguzi ndipo yapate leseni za LATRA" amesisitiza INSP. Kasongwa.

Naye Bw. Amani Mwakelebela, Afisa Mfawidhi LATRA Ifakara ameeleza kuwa kifungu cha (4)(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini sura ya 413 kinamtaka kila dereva anayeendesha chombo cha moto kibiashara awe amesajiliwa na kuthibitishwa na LATRA, hivyo ni wajibu wa madereva wa vyombo vunavyodhibitiwa na Mamlaka kufanya hivyo ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

"Dereva anapaswa kuthibitishwa baada ya kufanya mtihani wa kupimwa uelewa wake kwa kazi anazozifanya na akifaulu atapatiwa cheti na Mamlaka

*Inaendelea UK 22 >>>*

## LATRA YAPONGEZWA KWA KUSOGEZA HUDUMA KARIBU NA WADAU

*<<< Inatoka Uk 21*

kitakachoongeza wigo wa ajira kwani ataweza kuajiriwa ndani na nje ya mipaka ya Tanzania hususan katika Jumuia za Africa Mashariki. Tunasisitiza madereva mjitokeze kwa wingi ili kunufaika na fursa lukuki zinazopatikana baada ya kutahiniwa na kuthibitishwa na LATRA", ameeleza Bw. Mwakalebela.

Naye Bw. Ally Haji Dereva wa mabasi ya masafa marefu Ifakara ambaye amesajiliwa na LATRA amesema, "Naishukuru sana Serikali kwa kuiwezesha LATRA kufika Wilaya ya Kilombero mji mdogo wa Ifakara na kutufikishia huduma ambazo mwanzo ilitulazimu kuzifuata mjini Morogoro, lakini sasa zimefika karibu na tunazipata kwa urahisi na tutaendelea kuwakumbusha wenzetu ambao bado hawajathibitishwa ili wafanye hivyo."

Tangu Kuanzishwa kwa ofisi ya LATRA Wilaya ya Kilombero mji mdogo wa Ifakara Mkoani Morogoro mwezi wa sita mwaka 2024, mwitikio wa ukataji leseni za LATRA umeongezeka na wadau wa usafirishaji wakiwemo wamiliki na madereva wa vyombo vya moto kibiashara wamefanikiwa kutatua changamoto zao kwa wakati.

# WASAFIRISHAJI NA MADEREVA WAASWA KUZINGATIA SHERIA




*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA (wa katikati), Bw. Geofrey Silanda, Meneja Udhibiti Ubora na Usalama LATRA (wa kwanza kushoto) na Bw. Mbwana Ndaro, Afisa mfawidhi Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS- Center) (wa kwanza kulia) wakitoa tathmini fupi ya ukaguzi na udhibiti wa huduma za usafiri ardhini kipindi cha sikuku za mwisho wa mwaka 2024 kwa wanahabari ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam Januari 3, 2025.*

## WASAFIRISHAJI NA MADEREVA WAASWA KUZINGATIA SHERIA

<<< Inatoka Uk 22

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa rai kwa madereva na wamiliki wa mabasi kutii Sheria ya leseni za usafirishaji ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi na kuepuka ajali zinazogharimu uhai wa watanzania.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA Januari 3, 2025 alipotoa tathmini fupi ya ukaguzi na udhibiti wa huduma za usafiri ardhini kipindi cha sikuku za mwisho wa mwaka 2024.


Bw. Pazzy amesema, LATRA imebaini changamoto za ukiukwaji wa masharti ya leseni za usafirishaji kwa mabasi maalum ya kukodi maarufu kama Special hire ambapo baadhi yao yanabeba abiria mmoja mmoja wa kuokoteza na kukiuka sharti la leseni la kusubiri kukodiwa wakisingizia uhitaji mkubwa wa huduma kwa wakati huo, na pia wengine wanakiuka matumizi sahihi ya Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i-Button).

Aidha ameeleza kuwa, kwa sasa Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wanafanya ukaguzi maalumu katika vituo mbalimbali vya maeneo ya kimkakati na endapo watabaini uvunjifu wa Sheria, hatua stahiki zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

“Tumeanzisha kampeni maalum ya kutoa elimu na kuhakikisha mabasi haya yanafungwa Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD) na wanatumia kwa usahihi kitufe cha utambuzi wa dereva (i- Button) ili wakati wowote tuwatambue madereva wakiwa safarini. Pia, maafisa wetu wakishirikiana na mafundi wa VTD na Jeshi la Polisi wanafanya ukaguzi kwenye magari hayo,” amesema Bw. Pazzy.

Akitoa tathmini upande wa usafiri kwa njia ya reli, Bw Pazzy ameeleza kuwa huduma za usafiri wa treni ni nzuri ambapo usafiri wa treni ya kisasa (SGR) umerahisisha safari kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na kurudi kupitia Morogoro na reli ya kati imekuwa na usafiri wa treni hadi mara tatu kwa wiki kuelekea mikoa ya Moshi na Arusha.

Vilevile amesema, Mamlaka imeendelea kudhibiti na kutoa leseni maeneo yenye uhitaji zaidi ili kurahisisiha huduma za usafiri kwa watanzania na pia amewasihi kutumia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) https://pis.latra.go.tz/ kutambua mwendokasi wa basi na kutolea taarifa ya mabasi yanayotembea mwendo hatarishi kwa kupiga bure bila malipo siku zote kupitia namba 0800110019 au 0800110020.



SERA YA UBORA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 kwa lengo la kudhibiti usafiri ardhini kibiashara ikiwemo usafiri wa barabara, reli na waya.

Tumejizatiti kudhibiti huduma za usafiri ardhini kibiashara kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001 katika michakato yote inayohitajika ndani ya Mamlaka.

Sera yetu ya ubora ni kuendelea kutoa huduma zinazokidhi au kuzidi mahitaji na matarajio ya wateja wetu, wakiwemo watoa huduma zinazodhibitiwa, watumiaji huduma zinazodhibitiwa na wadau wengine.

Tunaendeleza ubora huu kupitia programu zinazomuwezesha kila mtumishi wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa usahihi kila wakati, kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusika, pamoja na viwango vya udhibiti, na malengo ya ubora ya QMS ISO 9001.

*Pamoja kwa Usafiri Bora*

CPA Habibu J. S. Suluo
MKURUGENZI MKUU
1 Julai 2024

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), likiongozwa na Bodi ya Wahariri**

Mwenyekiti: **CPA HABIBU SULUO** | Mhariri Mkuu: **SAMUEL KEENJA** | Wahariri Wasaidizi: **SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE** | Waandishi: **MAMBWANA JUMBE, NANCY AMANI** na **MARIAM NINA** | Wasanifu Jarida: **IBRAHIM SAID** na **DEUSDEDITY MASEMBA**

